MTIHANI WA KAMATI YA KUIMARISHA ELIMU KATIKA WILAYA ZA BARINGO KOIBATEK

102/2
KISWAHILI
KARASI YA 2
LUGHA
JULAI/AGOSTI
SAA : 2 ½

1. UFAHAMU.

Mabadiliko yaliyokumba jamii ya sasa ni ya kimkurupuko. Nasena hivi kwa sababu tunapoingalia jamii ya leo ninabaki kushangaa. Mimi sasa nina umri wa miaka 70 na nimeona mabadiliko mengi ya kuduwaza kabisa na hata ya kutisha.
Hebu tuchukue mfano wa nyanja mbalimbali. Elimu ya nyakati zetu ilikuwa ikitolewa kwa jamii kwa kufuata utaratibu wa umri mbalimbali. Elimu ya nyakati zetu ilikuwa ikitlewa kwa jamii kwa kufuata utaratibu wa umri mbalimbali. Elimu ya nyakiati zetu ilikuwa ikitolewa kwa jamii kwa kufuata utaratibu wa umri mbalimbali. Kwa hiyo mafunxo ya motto mdogo, kijana mwanamke, au watu wazimu, yalikuwa tofauti ingawaje yalikuwa na uhusiano.

Dhamira ya mafunzo haya ilikuwa kumwezesha kila mwanajamii kushiri katika harakati za maisha . Tulifunzwa jinsi ya kufanya shughuli kama vile ufugaji uvuvi, usukaji, hadithi na tanzu zingine za fasihi simulizi na mambo mengine muhimu. Kwa hivyo, lilikuwa jambo muhimu kwa watoto kufahamishwa mambo mengine muhimu na wavyele wao ili kuchukua hatamu wanapozeeka wavyele wao. Kwa mfano, watoto walifunzwa malishoni kuwatambua wanyama wa familia kwa alama mbalimbali. Hii ilikuwa muhimu yanachungwa pamoja.

Watoto pia walifunzwa kuhusu usukaji na kufinyanga, na nyanja zingine kuhusu maisha yao ya kila siku. Watoto wa kiume walifunzwa majukumu yao katika jamii huku wale wa kike wakifunzwa majukumu yao ambayo yalihusiana na maisha ya nyumbani. Fasihi simulizi husaidia sana kwani ilikuwa njia mojawapo ya kuwafunza watoto. Mafunzo haya yakitolewa jioni baada ya shughuli za mchana ili kuwaadibu vijana. Jioni ulikuwa wakati mwafaka kwa kuwa kila mtu alikuwa amemaliza kazi. Aidha, wazazi hakutaka watoto na vijana kutembeatembea usiku na kujihasiri. Pia wazazi hawakuwa na nafasi mchana kukutana na watoto wao kwa sababu za tumbo!

Lakini siku hizi, mambo ni mengine. Kwanza, shule hizi zilizoletwa na mzungu zimebadili weupe kuwa weusi! Watoto siku hizi huchukua tasriban asilimia 90 ya

maisha yao shuleni wakiwa na walimu. Watapata wapi muda wa kuzungumza na wazazi wao? Wakati huohuo kinaya ni kwamba hata wakati watoto wako wako nymbani, wazazi nao hawana muda wa kufanya kazi yao! Eti shughuli **zimewasakama** kiasi cvha kutojumudu.
Nani atawafanyia uzazi wa kukopa/ Matokeo ya **sintofahamu** hii ni ya kusikitisha. Shule zimekumbwa na matatizo mengi kwa kuwa watoto hawashauriwi na wazazi wao tena. Fujo, wizi utumiaji wa madawa ya kulevya na mauaji vimekuwa ndiyo kawaida katika baadhi ya kufundisha masomo ya kwawaisa na kufanya kazi ya kuwashuri wanafunzi kikamilifu bila wazazi kufanya kazi yao ipasavyo nyumbani. Tusisahau kuwa walimu pia ni wazazi na wanahitaji kuwashauri watoto wao.

Sasa, swali ambalo mini hujiuliza ni hili; shule zimesaidia kwa njia gain? Kuleta matatizo haya yote ama kuyatatua?

Katika haya yote, linalonisikitisha kama mzee ni tabia ya vijana wa siku hizi. Kizaazaa cha siku hizi ni vijana kuvua adabu kabisa. Shuleni kwenyewe, utakuta baadhi ya vijana walifanya mambo ya kushangaza. Kuna hii mbinu mpya ya kutumia madawa ya kulevya ambayo imewafanya baadhi ya vijana kuwa mgofu ya watu. Hali hii imewafanaya wengine kuzusha fujo shuleni na kuharibu mali. Wengine wanakosa kufuata ushauri wa walimu wao huku wengine hata wakiwatusi. Wanasahau ushauri wa wahenga kuwa usitukane wakunga na uzazi ungalipo.

Ninapotembelea baadhi ya miji nchini, hutaka kufunga macho lakini nahofia magari kunigonga! Vijana wanatembea wakiwa wanaonyesha maungo yao na kuwa uchi kabisa eti kuiga mitindo ya Ulaya. Wengine wameingilia kufanya mapenzi ovyo. Vijijini pia vijana wamepotoka. Hata salamu za Mungu wanawauzia wazee. Matokeo? Watoto kuzaa watoto, watoto, watoto wasio na hahitaji ya kila siku na sasa vijana wengi wemeumwa n zimwi. Kutowajibika kwa namna hii miongoni mwa viongozi wa kesho(au ni wa leo?) ni maangamizi . Ikiwa maendeleo ndiyo haya, basi kitumbua kimeingia mchanga!

Siku zetu, mambo yalikuwa shwari, Mambo yalitendeka kwa utaratibu. Lakini si sasa. Hatuwezi kurudi nyuma, ndiyo. Lakini kama huku ndiko kwenda mbele, moyo wangu umejaa wasiwasi. Vijana wanaweza kuchukua msimamo wa kurekebisha mambo yaliyoharibika. Mimi nimezeeka na karibuni, nitarudi mavumbini,. Je, mtachukua jukumu la kuufanya ulimwengu uwe bora kwa tabia zenu njema?

Maswali

(a) Ni nini dhamira ya mwandishi wa makala haya? (alama 1)
(b) msemaji anadai kuwa mabadiliko yanayoikumba jamii ya kisasa ni ya ‘kimburupuko’. Fafanua (alama 2)
(c) Kuna mambo gain katika taarifa yanayothibitisha kuwa shule zilizoletwa na Mzungu “imebadilika weupe kuwa weusi”?
(d) (i) kwa nini wazazi wa jadi waliwatambia watoto hadithi majira ya jioni? (alama 2)
(ii) hali hii iliwasaidiaje hawa watoto? (alama 2)

(e) "Wazazi wa siku hizi na walimu ndio wanaopaswa kulaumiwa kwa kutovuka kwa nidhamu miongoni mwa vijan." Thibitisha. (alama 2)
(f) Nakili tamathali zozote mbili za lugha zilizotumiwa katika taarifa (alama 2)
(g) eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika taarifa. (alama 2)

(i) kuwaadibu
(ii) Zimewasakama
(iii) Sintofahamu
(iv) Magofu ya watu

2.MUHTASARI
UFUPISHO
Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali.
Leo hii, baadhi ya ndoa zimo hatarini kwa sababu wanaume wengi wamekiuka uume. Wametua mizigo ya maisha waliyopewa kubeba na kutwika kwa wake zao. Wanaume alidhamiriwa kuwa mume katika ndoa na baba katika familia. Tabia za baadhi ya waume wa leo zimedidimisha matumaini ya wake zao na kudhoofisha nyoyo za wanao. Wameingiwa na uchoyo, uroho na tama.

Wanaume wengine wana mazoea ya kula hotelini au kwenye kumbi za starehe bila hata haya machoni wakifahamu waziwazi kwamba mke na watoto nyumbani hawana nata maji ya supu kwenye kigae. Hufanya hivyo kutokana na namna wanavyoogopa gharama ya malezi na hivyo huamua kutelekeza familia zao.

Wakati ni sasa kwa wanaume kugeuza vipaumbele, fikira, umuhimu na madhaumuni maishani ili yalingane na mahitaji ya familia zao. Mume kamili huafakari matatizo, mapenzi na mashaka ya familia. Hujishughulisha kwa dhati ili kukuza na kudumisha upendo ndani ya familia kwani yeye hutegemewa. Hufanya juu chini kuwarejeshea raha, matumaini ya maisha mema na tabasamu usoni. Anapofanya nivyo, ufahamu daima dawamu kuwa hakuna aliyemshurutisha au kumlazimisha bali ametendea wema wale walio wema kwake.

Ni dhahiri kuwa sote twaandamwa na uchochole. Si vyema mume kuwa na fikra finyu zinzokuwa tama za anasa na ulevi usiofaidi yeyote. Lengo kuu la ndoa ni kuchukuliana mzigo. Mke na mume hawana budi kufuhaia raha na kuvumilia shida pamoja. Ihsani na utu view vitangulizi katika matendo ya mume. Waume wajitahidi kudumisha ndoa zao kwa maana ndoa ndiyo mlinzi wa jamii staarabu na ni chanzo cha amani moyoni na maadili ya kudumu.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa, fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 45-50)

(alama 4)

Nakala awali

Nakala safi.

(b) Fupisha haya mbili za mwisho (maneno 70-80) (alama 8)

Nakala awali

Nakala safi.

3.**MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia visisitizi. (alama 2)
Mitume hao walivuka mito hiyo.

(b) Ainisha aina za nomino katika sentensi hii: (alama 2)
(i) Genge la wezi limewaangaisha watu wa Kilifi.
(ii) Kuimba kwake kulifurahisha

(c) Sahihisha sentensi zifuatazo: (alama 2)
(i) Mjomba alinipea zawadi dada ya kupita mtihani.
(ii) ubao chenye umeanguka umeharibika

(d) Andika kwa wingi: (alama 1)

(e) Tunga sentensi kwa kutumia nomino zifuatazo na kivumishi –ingi. (alama 2)
(i) Viroboto
(ii) Pesa

(f) (i) eleza maana ya viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsi viambata (alama 2)
(ii) Toa mfano mmoja wa kiwakilishi nafsi huru na kiwakilishi nafsi kiambata. (alama 1)

(g) Jaza nafsi zilizoachwa;

KITENZI	NOMINO
Hesabu	
Ajiri	

(h) Tumia neon “haraka’ kama: (alama 2)
(i) Taja sauti mbili za kaakaa gumu: (alama 2)
(j) Andika katika kauli ya kutendesheka (alama 1)
Ni rahisi kupunguza maji hayo.
(k) Bainisha aina za vielezi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) mutual ameelekea kwao.
(ii) Mvua itanyesha tena.
(h) fanaua miundo yoyote mitatu ya monimo katika ngeli ya;
a-wa (alama 3)
(i)
(ii)
(iii)
(m) Tumia viakifishi vifuavyo kutungia sentensi sahihi: (alama2)
(i) Ritifaa
(ii) Parandesi

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielezo cha mistari: (alama 3)
Mtoto aliyechezea moto jana aliuma sana.
(o) andika katika usemi wa taarifa:
“Ninakutembelea ikiwa nitaweza,” Chebet alitamka. (alama 2)
(p) Eleza tofauti kati ya kirai na kishazi (alama 2)
(q) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendea (alama 2)
(i) La
(ii) Kua
(r) Tunga sentensi ili kuonyesha tofauti kimaana katika jozi hili: (alama 2)
Tega
Teka
(s) eleza matumizi ya ‘kwa’ na ‘ku’ katika sentensi hizi: (alama 3)
Eleza matumizi ya “kwa’ na katika sentensi hizi; (alama 3)
(i) mwalimu anakuita.
(iii) Kucheka kwake kunaudhi.

4**. ISIMU JAMII**

(a) eleza nini maana ya isimujamii (alama 2)

(b) fafanua jinsi “ hali ya mtu” inavyoathiri namna anavyoweza kutumia lugha katika mazingira Fulani. (alama 4)

(c) Eleza sifa zozote nne za mazungumzo katika mazingira rasmi.
(alama 4)